HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO MHESHIMIWA DKT. ASHA-ROSE MIGIRO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2005/2006

I. HOJA

1. Mheshimiwa Spika, baada ya taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, iliyochambua Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako tufuku lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

II. UTANGULIZI

2. Mheshimiwa Spika, naomba nianze hotuba yangu kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kuweza kuliongoza taifa letu kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 1995 hadi mwaka huu anapomaliza muda wake. Katika kipindi hiki, ameonyesha umahiri mkubwa wa uongozi katika nyanja zote za maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na mambo mengine, uongozi wake umewezesha uchumi wa nchi yetu kukua kutoka asilimia 4 mwaka 1995 hadi asilimia 6 mwaka huu, huduma za kijamii zimeendelea kuimarika na miundo mbinu imekuwa bora zaidi. Hali kadhalika, kwa jitihada hizo hivi sasa nchi yetu ni moja ya nchi zilizo katika orodha ya kupunguziwa sehemu ya deni lake la nje kutokana na kuwepo kwa mfumo imara wa utawala bora.

3. Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed

Shein, kwa juhudi zake kubwa za kumshauri Mheshimiwa Rais na za kuimarisha Muungano na kwa kuhamasisha utekelezaji wa Sera mbali mbali za nchi yetu.

4. Mheshimiwa Spika, kwa uzito huo huo, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Waziri Mkuu na Mbunge wa Hanang, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji na Mbunge wa Handeni, na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha na Mbunge wa Rombo kwa hotuba zao nzuri zilizotoa mwelekeo wa hali ya uchumi na Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2005/2006. Malengo, maelekezo na vigezo vilivyomo kwenye Hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2005/06.

5. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka kumi, wewe, Mheshimiwa Spika, umeonyesha uhodari mkubwa katika kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge. Nachukua nafasi hii kukupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu tukufu kwa utulivu na hekima kubwa. Nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti kwa kuliongoza Bunge wakati ulipokuwa na majukumu mengine nje ya Bunge.

6. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa kupitia CCM. Tunamtakia kila la kheri na wana-CCM tunamhakikishia ushindi mkubwa katika uchaguzi ujao. Vile vile nampongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa mgombea kiti cha Urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi.

7. **Mheshimiwa Spika**, napenda sasa kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Sophia Simba (Mb), na Makamu wake Mheshimiwa Haroub Masoud, Mbunge wa Koani, kwa kutuongoza vizuri na kutushauri kwa makini katika kipindi chote cha miaka mitano. Tunaishukuru Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuichambua na kuijadili kwa kina bajeti yetu ya mwaka 2005/06 kabla ya kuiwasilishwa hapa Bungeni. Ushauri uliotolewa na Kamati hiyo umesaidia sana kuboresha bajeti hii. Tunaishukuru sana Kamati hii kwa kuiwezesha Wizara kuongezewa kiwango cha fedha ya bajeti. Haya ni matokeo ya jitihada na mchango wa mawazo na maelekezo yao.

8. Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuungana na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi na pole kutokana na vifo vya wabunge wenzetu kadhaa vilivyotokea katika kipindi kifupi kilichopita. Wabunge hao ni: Hayati Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Hayati Mheshimiwa Theodos James Kasapira (Mb), aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Hayati Mheshimiwa Frank Michael Mussati (Mb), aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Hayati Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria (Mb), aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo, Hayati Mheshimiwa Abubakar Towegale Kiwanga (Mb), aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na Hayati Mheshimiwa Margaret Bwana (Mb), aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hawa mahali pema peponi. Amin. Aidha, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliopatwa na misiba, waliouguliwa au waliopata matatizo mengine ya kijamii. Naomba Mwenyezi Mungu awape tahfifu.

9. Mheshimiwa Spika, napenda sasa kutoa maelezo ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu katika muktadha wa dhamana ya Wizara

yangu, na baadaye kufanya mapitio ya utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2004/05, na makusudio ya utekelezaji katika kipindi cha mwaka 2005/06.

III. MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA TATU

10. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Wizara yangu imepata mafanikio makubwa chini ya uongozi wa Jemedari wetu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Mafanikio haya yanatokana na Ilani ya Uchaguzi za miaka ya 1995 na 2000, na utekelezaji wa Sera sahihi za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi.

11. Mheshimiwa Spika, kabla ya Serikali ya Awamu ya Tatu kuwa madarakani mwaka 1995, Wizara yangu ilikuwa na Sera moja ya Wanawake katika Maendeleo iliyopitishwa mwaka 1992. Katika kipindi cha Awamu ya Tatu, Wizara imefanikiwa kuandaa Sera nne ambazo ni:- Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996), Sera ya Maendeleo ya Mtoto (1996), na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) iliyochukua nafasi ya Sera ya Wanawake katika Maendeleo na hivi sasa Wizara imekamilisha maandalizi ya rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Familia (2005).

Maendeleo ya Jamii

12. Mheshimiwa Spika, maudhui ya Sera ya Maendeleo ya Jamii ni ushiriki wa watu katika kuibua, kupanga, kutekeleza na kufanya tathmini ya mipango yao ya maendeleo. Aidha, Sera inasisitiza umuhimu wa kuwawezesha wananchi kupata maarifa na stadi mbali mbali zitakazowawezesha kushiriki kikamilifu katika kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi ili kuongeza tija na kujiletea maendeleo

yao. Hali kadhalika Sera inatoa kipaumbele kwenye matumizi ya mbinu shirikishi na teknolojia sahihi kwa madhumuni ya kupunguza mzigo wa kazi, hasa kwa wanawake, na kuongeza tija kwa ujumla.

13. Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, madhumuni makuu ya Sera ya Maendeleo ya Jamii ni kuwawezesha wananchi mmoja mmoja, katika familia, vikundi au jumuiya kuchangia zaidi katika azma ya Serikali ya kuleta maendeleo kwa njia ya kujitegemea kuanzia ngazi ya kijiji na mkoa, hatimaye Taifa kwa ujumla. Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii umeleta ongezeko la ushiriki wa wananchi katika kufanya maandalizi ya miradi na programu mbalimbali na kuzitekeleza. Kutokana na ushiriki wao, wananchi sasa wamejihusisha kikamilifu katika mchakato wa maendeleo, wanamiliki miradi inayotekelezwa na hivyo kuifanya kuwa endelevu. Hii imejidhihirisha katika utekelezaji wa programu na miradi ya sekta mbali mbali.

14. Mheshimiwa Spika, programu zilizotekelezwa kwa mafanikio ni pamoja na Mpango wa Afya kupitia Maji na Usafi wa Mazingira (HESAWA), Mpango wa Uhai, Ulinzi na Maendeleo ya Mtoto, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), miradi ya maji vijijini, ujenzi wa nyumba bora na utayarishaji wa programu za mafunzo na elimu ya Mipango Shirikishi jamii. Kutokana na mafanikio hayo Serikali za Mitaa zimeamua kutumia mbinu shirikishi katika kuandaa na kutekeleza mipango yote ya maendeleo.

15. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005, Wizara yangu imedurusu na kuongeza mitaala ya mafunzo yatolewayo katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na vya Maendeleo ya Wananchi ili kukidhi mahitaji ya soko na changamoto mbali mbali za maendeleo. Aidha Wizara imeendelea kuboresha majengo na miundo mbinu katika

vyuo hivyo ili kuimarisha mazingira ya kujifunzia. Katika jitihada hizo, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kimepatiwa chanzo cha maji cha kuaminika zaidi.

16. Mheshimiwa Spika, ndani ya kipindi hiki, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya aina mbili katika vyuo vyake vya maendeleo ya jamii. Aina ya kwanza ni Vyuo vinavyotoa mafunzo ya Cheti na Stashahada ya Juu katika fani ya Maendeleo ya Jamii, na aina ya pili ni vile vinavyotoa mafunzo ya Maarifa na Stadi mbali mbali za kuwawezesha wananchi kujitegemea. Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kinatoa Stashahada za Juu katika fani za Maendeleo ya Jamii, Upangaji na Utekelezaji wa Mipango Shirikishi na Jinsia na Maendeleo. Chuo hicho kimesajili wanafunzi 228 mwaka 2003/04 ikilinganishwa na wanafunzi 53 mwaka 1995/96. Vyuo vinavyotoa mafunzo ngazi ya Cheti ambavyo ni Buhare, Missungwi na Rungemba vimeweza kusajili wanafunzi 209 mwaka 2003/04 ikilinganishwa na wanafunzi 71 mwaka 1995/96. Aidha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 58 vimeendelea kutoa mafunzo ya Maarifa na Stadi mbali mbali na viliweza kuwapatia mafunzo wananchi 23,086 mwaka 2003/04 ikilinganishwa na wananchi 3,942 mwaka 1995/96. Ongezeko hili linatokana na ari ya wananchi, hususan wanaoishi karibu na maeneo ya vyuo hivi, kutaka kupata elimu na ufahamu zaidi wa masuala ya maendeleo.

17. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeandaa na kuzindua Mkakati wa Kuwakinga Wanawake na Watoto Dhidi ya UKIMWI na Magonjwa ya Zinaa. Mkakati huo, unatekelezwa na wataalam katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika Sekretarieti za Mikoa na katika Halmashauri kwa kushirikisha wananchi. Mkakati huu umeongeza uelewa wa masuala ya UKIMWI katika jamii, na hasa namna ya kuwakinga wanawake na watoto dhidi ya maambukizi. Aidha, Wizara imeunda

kamati ya UKIMWI na kutoa mafunzo yanayohusu UKIMWI kwa watumishi 477 kutoka makao makuu ya Wizara na vyuo vya Wizara.

Maendeleo ya Wanawake na Jinsia:

18. Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000, ina madhumuni ya kutoa miongozo mbali mbali itakayohakikisha kuwa Sheria, Sera, Mikakati na Mipango ya maendeleo yote hapa nchini inazingatia usawa wa jinsia. Katika kutekeleza hilo, Wizara yangu ilianzisha Dawati la Jinsia (Gender Desk) katika kila Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri ili kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia siyo tu yanazingatiwa bali matokeo ya kuleta usawa yanapatikana. Aidha Watendaji wa Dawati hilo wamepewa mafunzo ya mbinu na stadi za kuzingatia jinsia katika utayarishaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa sera, programu na miradi pamoja na Sera za kijumla kama vile Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

19. Mheshimiwa Spika, katika kuwawezesha na kuwaimarisha wanawake kiuchumi, Wizara yangu imewezesha utoaji wa kutoa mikopo kwa makundi mbali mbali ya wanawake. Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Wizara ilianzisha Mifuko miwili ijulikanayo kama Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (WDF) na Mtaji wa Uzalishaji Mali kwa Wanawake (CREW-T) kwa ajili ya kutoa mikopo nafuu na wanawake wengi wamejitokeza kuchukua mikopo hii. Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake umeweza kuwapatia mikopo wanawake 28,302 mwaka 2003, ikilinganishwa na wanawake 757 mwaka 1996/97, hili ni ongezeko kubwa. Aidha mtaji wa WDF ulioanza na shilingi 241,400,000 mwaka 1996 ulifikia shilingi 1,499,925,000 mwaka 2004/05. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, kumewahamasisha wanawake wengi kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali, ambavyo

vimeongezeka kutoka 1,207 mwaka 2000 hadi kufikia 4,940 mwaka 2004. Vile vile wanawake wengi wamejiunga na Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa na SACAS. Aidha, mtaji wa Uzalishaji Mali kwa Wanawake Tanzania umewakopesha wanawake 6,002 mwaka 2003 ikilinganishwa na wanawake 1,551 waliokopeshwa katika kipindi cha mwaka 1995. Wizara pia kwa kushirikiana na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote na wadau wengine umewawezesha jumla ya wanawake 1,422 kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam. Mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa wanawake waliojishughulisha kiuchumi ni pamoja na kupata masoko, kuongeza ubora wa bidhaa zao na kupunguza umaskini wa kipato.

20. Mheshimiwa Spika, ili ziwape wanawake uwezo wa kisheria katika kupata na kutetea haki zao, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba pamoja na wadau wengine, ilibainisha sheria zilizoonekana kuwanyima wanawake na watoto haki, usawa na maendeleo kwa lengo la kuzifanyia marekebisho. Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998 imewawezesha wanawake kutumia sheria hiyo kudai haki zao na kujitokeza kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola mara wanapofanyiwa ukatili dhidi yao. Aidha baadhi ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake kwa mfano mauaji ya wanawake wazee yamepungua kutoka 371 mwaka 2000 kufikia 304 mwaka 2003. Marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi za Vijiji ya mwaka 1999 yamewawezesha wanawake kupata haki sawa katika milki na matumizi ya ardhi na kupata fursa za kiuchumi. Aidha sheria hizi zimeiwezesha jamii kuwa na mtazamo wa kuheshimu utu na haki za wanawake. Hivi sasa Serikali inaendelea na juhudi zake za kupitia sheria mbalimbali kwa lengo la kuziboresha.

21. Mheshimiwa Spika, ingawaje kumekuwepo na mafanikio katika maeneo mbali mbali, bado kuna changamoto kubwa zinazotokana na

kujikita kwa mfumo dume katika jamii unaosababisha jitihada za kuleta usawa wa jinsia zisifanikiwe. Kwa mfano kuwepo kwa mfumo dume katika baadhi ya mila na desturi kunadhoofisha haki za wanawake na watoto. Mfumo dume katika upatikanaji wa elimu, ajira, kupandishwa vyeo na katika kupunguza wafanyakazi, umeathiri ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi. Wanawake wengi wamejikuta wakikatishwa tamaa katika jitihada zao za kujikomboa kutokana na athari za mfumo dume. Hili ni eneo mojawapo ambalo Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa aliagiza lifanyiwe kazi, akiwahutubia wanawake wapatao 10,000 walioandamana wakati wa kuadhimisha Miaka Kumi ya Azimio na Ulingo wa Beijing huko Dar es Salaam, Machi 8 mwaka huu.

22. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ushiriki wa wanawake katika vikao vya maamuzi na utendaji, idadi ya wanawake katika masuala ya siasa na katika ngazi za kutoa maamuzi imeongezeka. Uwakilishi wa wanawake Bungeni umeongezeka kutoka asilimia 17.5 mwaka 1995 hadi kufikia asilimia 22.5 mwaka 2004. Vile vile hadi mwaka 2004 uwakilishi katika Mabaraza ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji umefikia asilimia 33.0 kutoka asilimia 25 mwaka 1995 na idadi ya Mawaziri Wanawake imeongezeka kutoka asilimia 11.1 mwaka 1995 hadi kufikia asilimia 14.8 mwaka 2004. Katika ngazi ya utendaji idadi ya Makatibu Wakuu imeongezeka kutoka mmoja mwaka 1995 hadi kufikia saba mwaka 2004.

23. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matukio ya kimataifa, maadhimisho ya miaka kumi ya Azimio na Ulingo wa Beijing ya mwaka 2005 yalifanyika kwa kishindo kikubwa ndani na nje ya nchi. Hapa Tanzania, maadhimisho haya yalikuwa na umuhimu wa pekee, kwani yalitumika kufanya mapitio ya utekelezaji wa miaka kumi wa Azimio na

Ulingo wa Beijing na tathmini ya utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tatu katika kipindi cha miaka kumi. Aidha, wanawake wa Dar es Salaam walitumia fursa hiyo kumshukuru Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa jitihada zake za kuleta usawa wa jinsia katika kipindi chote cha uongozi wake kilichokwenda sambamba na miaka kumi ya utekelezaji wa Azimio hili. Nachukua nafasi hii kama Waziri mwenye dhamana ya Maendeleo ya Wanawake hapa nchini, kwa niaba ya wanawake wote wa Tanzania, kutoa shukrani za pekee kupitia Bunge lako tukufu kwa Mheshimiwa Rais. Jitihada zake za kuhakikisha kuwa kiwango cha usawa wa jinsia kimepanda katika maeneo yote ya kisiasa na kiutendaji katika kipindi chake zimeweka msingi mzuri kwa hatua zaidi kupigwa katika awamu ya nne ya Serikali yetu.

24. Mheshimiwa Spika, kutokana na uhamasishaji uliofanyika wakati wa maandalizi na maadhimisho ya miaka kumi ya Azimio na Ulingo wa Beijing, wadau mbali mbali walijitokeza kushirikiana na Serikali katika kushughulikia masuala ya wanawake. Chama cha Madaktari Wanawake (MEWATA) kiliendesha zoezi la kupima matiti ambapo jumla ya wanawake 7,259 walijitokeza na kati yao 757 walikutwa na uvimbe. Kati ya wale waliokutwa na uvimbe, 34 waligundulika kuwa na saratani ya matiti na hivi sasa wanapata matibabu zaidi. Shughuli nyingine katika maadhimisho hayo ilikuwa ya kuwasha mishumaa kama ishara ya kuwakumbuka wanawake walioathirika au kufa kutokana na UKIMWI. Shughuli hii iliongozwa na Chama cha Wanawake wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (NETWO+). Vile vile yalifanyika maonesho ya biashara ya bidhaa zinazozalishwa na wanawake, makongamano mbali mbali yaliyoendeshwa na Wizara, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za elimu ya juu. Chama cha Wataalam wa Kilimo Wanawake kilisambaza mbegu za mihogo na kutoa elimu ya upandaji wa mbegu hizi kwa Wanawake wa Halmashauri ya Mkuranga. Hatimaye maandamano ya

wanawake yalifanyika siku ya kilele tarehe 8 Machi, 2005 na kupokewa na Mheshimiwa Rais. Nachukua nafasi hii kupitia Bunge lako tukufu kuwashukuru wale wote walioshirikiana nasi katika kufanikisha maadhimisho haya. Kwa namna ya pekee nawashukuru sana wenyeji wa sherehe hizi kitaifa Mheshimiwa Luteni (Mstaafu) Yusuf Makamba na viongozi wenzake wa Mkoa wa Dar Es Salaam na wananchi wote kwa mchango wao mkubwa katika maadhimisho hayo. Aidha naishukuru mikoa yote kwa kuadhimisha siku hii.

25. Mheshimiwa Spika, kimataifa maadhimisho haya yalifanyika tarehe 8 Mwezi Machi, 2005 huko New York Marekani wakati wa kikao cha Kamisheni ya Hali ya wanawake. Kikao hiki kilikuwa na ajenda moja kuu ya kutathmini utekelezaji wa Ulingo na Azimio la Beijing katika ngazi ya kimataifa na kupendekeza mipango ya baadaye ili kuleta usawa, amani na maendeleo. Tathmini hiyo imeonyesha kuwa bado kuna vikwazo vingi vya kimaendeleo kwa wanawake katika nchi nyingi. Kutokana na hali hii kikao kiliazimia kwamba utekelezaji wa Ulingo wa Beijing uendelee kwa kasi kubwa zaidi, na ufanyike kwa kuzingatia Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW), Malengo ya Maendeleo ya Millenia na Mipango inayohusu kupunguza maambukizi ya UKIMWI, hasa kwa wanawake.

26. Mheshimiwa Spika, jitihada zinazofanywa za kuingiza masuala ya jinsia katika shughuli mbali mbali zimefanya harakati za kuleta uwiano wa kijinsia na masuala yanayohusu wanawake na jinsia kuwa ajenda muhimu katika mikutano ya kitaifa na kimataifa, Tanzania ikiwa mstari wa mbele. Mfano mzuri ni Mkutano wa Kimataifa wa Wakuu wa Nchi za Maziwa Makuu kuhusu Amani, Usalama, Demokrasia na Maendeleo uliyofanyika hapa nchini mwezi Novemba, 2004. Katika kikao hicho Tanzania iliwezesha masuala ya jinsia kuingizwa katika Tamko la Dar Es

Salaam lililotolewa na Wakuu wa Nchi hizi. Tamko hilo lilizingatia Azimio la Umoja wa Mataifa Namba 1325 linalozitaka nchi za Umoja wa Mataifa kuendeleza amani na utulivu kwa kukomesha migogoro na vita kati ya nchi na nchi na katika familia. Kipengele muhimu cha Azimio hili ni ushiriki wa wanawake katika kusuluhisha na kukomesha migogoro na vita. Sambamba na kikao hicho, Wake wa Marais wa Nchi za Maziwa Makuu walikutana na kubainisha nafasi zao katika kuleta amani na maendeleo. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mama Anna Mkapa kwa kuwa mwenyeji wa kikao hicho ambacho kiliwezesha Wake wa Marais kushiriki katika mchakato wa kuleta amani ndani ya nchi za Maziwa Makuu. Vile vile walipata nafasi ya kubadilishana uzoefu katika kutekeleza miradi yenye lengo la kuinua hali za wanawake na watoto.

27. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kuratibu Mfuko wa Mafunzo kwa Wanawake Tanzania (TFTW) uliotekelezwa kuanzia mwaka 1989 hadi 2003 kwa ushirikiano na Serikali ya Canada. Madhumuni ya Mfuko huo yalikuwa ni kuinua viwango vya elimu kwa wanawake ili waweze kuongeza uwezo wao na kushiriki katika siasa na vyombo vya kutoa maamuzi katika ngazi mbali mbali. Katika kipindi hicho Mfuko uliwasomesha jumla ya wanawake 2,076, kati ya hao, 309 katika masomo ya muda mrefu, 1,750 mafunzo ya muda mfupi, na 17 mafunzo ya kushikizwa.

28. Mheshimiwa Spika, kutafsiriwa kwa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 katika Kiswahili chepesi kumeongeza ufahamu na uelewa wa idadi kubwa ya jamii kuhusu masuala mbali mbali ya wanawake na jinsia kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha Wizara iliandaa Mpango wa Kitaifa kuhusu Kutokomeza Aina Zote za Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto na kuusambaza kwa wadau. Mpango huo unaendelea kutekelezwa ambapo jamii sasa imehamasika na kutoa taarifa za matukio ya ukatili dhidi ya wanawake

na watoto kwenye vyombo vya sheria. Vile vile Tanzania imeridhia Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (Optional Protocol to CEDAW). Itifaki hii inatoa fursa kwa wanawake kutoa malalamiko yao moja kwa moja kwenye Kamati ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW).

Maendeleo ya Mtoto

29. Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 1996 inatoa dira kuhusu uhai, ulinzi na maendeleo ya mtoto. Aidha Sera inalenga kuwashirikisha watoto katika ujenzi wa Taifa pamoja na kuwakinga dhidi ya maradhi mbali mbali. Katika kutekeleza mpango wa uhai, ulinzi na maendeleo ya mtoto, jamii imehamasika na kuweza kujitokeza katika kuwapeleka watoto wao kliniki kupata chanjo za msingi. Chanjo hizo ni Polio, Surua, Pepopunda, DPT/HB na Kifua Kikuu. Aidha kumekuwa na ongezeko la watoto waliopata chanjo kwa ajili ya kinga ya magonjwa mbali mbali kwa kipindi cha mwaka 1995 – mwaka 2003 kama ifuatavyo:-

(i) Polio kutoka asilimia 79 mwaka 1995 hadi asilimia 92 mwaka 2003;
(ii) Surua kutoka asilimia 76 mwaka 1995 hadi asilimia 90 mwaka 2003;
(iii) DPT/HB kutoka asilimia 82 mwaka 1995 hadi asilimia 88.5 mwaka 2003;
(iv) Kifua Kikuu kutoka asilimia 88 mwaka 1995 hadi asilimia 94.5 mwaka 2003 na
(v) Pepopunda kutoka asilimia 30 mwaka 1995 hadi asilimia 83 mwaka 2003.

30. Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 1995 – 2004 Serikali iliridhia na kutekeleza Mikataba na Itifaki zifuatazo za kimataifa kuhusu Maendeleo ya Watoto:-

(i) Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto;

(ii) Itifaki za nyongeza ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto kuhusu Biashara ya Kuuza Watoto na Upigaji Picha za Udhalilishaji watoto.

(iii) Itifaki ya Nyongeza ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto kuhusu ushirikishwaji wa Watoto kwenye migogoro ya Kivita.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na hatua hii ni pamoja na kuweka mazingira mazuri kitaifa ya utoaji wa haki za watoto na kuhakikisha ustawi wao. Kwa kuridhia mikataba na Itifaki hizi Tanzania imeungana na nchi nyingine za Umoja wa Mataifa katika jitihada za kuwapatia watoto haki zao.

31. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita haki za watoto zimefahamika zaidi kwa jamii na watoto wenyewe. Aidha vyombo vifuatavyo vimeanzishwa ili kuwashirikisha zaidi watoto katika kufanya maamuzi yanayogusa haki na maslahi yao:-

(i) Mtandao wa Harakati za Watoto Tanzania (Tanzania Movement for and with Children – TMC) uliozinduliwa tarehe 28 Aprili, 2001;

(ii) Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Desemba, 2002.

Aidha mtandao wa Tanzania wa Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Utotoni (Tanzania Early Childhood Development Network) umeundwa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa watoto wadogo wanapata msingi mzuri wa

malezi bora. Vile vile tawi la Tanzania la mtandao wa kutokomeza ukeketaji la Kanda ya Afrika Mashariki limeanzishwa ili kuimarisha mapambano dhidi ya mila zinazoleta madhara kwa watoto hususani ukeketaji. Taarifa tulizonazo ni kwamba ngariba wengi wameanza kuachana na mila hii yenye madhara.

32. Mheshimiwa Spika, katika kipinndi hicho Serikali ilianzisha Idara ya Maendeleo ya Mtoto katika Wizara kwa lengo la kutekeleza kikamilifu Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mtoto. Kuundwa kwa Idara hii kumewezesha masuala yanayohusu maendeleo na ustawi wa mtoto kuangaliwa kwa umakini zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine ilifanya mapendekezo ya kurekebisha sheria mbali mbali zinazohusu haki za mtoto na kuweza kuingiza masuala ya watoto kwenye mwongozo wa MKUKUTA na maandalizi ya bajeti ya kila mwaka.

Utawala na Utumishi

33. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuzingatia misingi ya utawala bora katika uendeshaji na utoaji huduma zake kwa walengwa. Mpango Mkakati ulioandaliwa na Wizara yangu unahakikisha ubora wa huduma zinazotolewa na Wizara kwa kuzingatia nafasi na rasilimali zilizoainishwa. Aidha, watumishi wakiwemo viongozi wa ngazi za juu walipewa mafunzo kwa nia ya kuimarisha utawala na kuziba mianya ya rushwa.

34. Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 1995 na 2005 Wizara yangu imewawezesha watumishi 398 kwa kuwapatia mafunzo ya kimenejimenti na kitaaluma. Kati ya watumishi hawa 31 wamepata stashahada ya uzamili na wawili wamepata udaktari wa falsafa. Aidha Maafisa Maendeleo ya Jamii 205 na waalimu 898 walipandishwa vyeo kwa utaratibu wa mserereko. Katika kipindi hicho Wizara ilipata nafasi 414 za ajira mpya. Hatua hizo zimewezesha Wizara yangu kujaza nafasi zilizokuwa wazi na pia kuimarisha utendaji kazi ndani ya Wizara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara.

IV. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2004/05:

35. Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa maelezo ya mapitio ya utekelezaji wa bajeti na mpango wa mwaka 2004/05.

Maendeleo ya Jamii

36. Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako tukufu kwamba Wizara yangu ingetathmini utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996 ili kubaini mafanikio na upungufu. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa tathmini hiyo imefanyika katika Mikoa ya Iringa, Kigoma, Manyara, Mwanza, Morogoro na Ruvuma. Masuala muhimu yaliyojitokeza kutokana na tathmini hiyo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Dhana ya ushiriki wa wananchi na matumizi ya mbinu shirikishi (participatory approaches) katika shughuli za kujiletea maendeleo yao, ambayo ndiyo msingi wa Sera ya Maendeleo ya Jamii, imeeleweka vema zaidi kwa wananchi.

Matokeo yake ni utekelezaji mzuri ambao umeleta mafanikio makubwa katika miradi ya maendeleo hasa katika ngazi ya kijiji. Hii inajidhihirisha katika utekelezaji wa programu na miradi mbali mbali kama TASAF, MMEM, HESAWA, miradi ya maji vijijini na ujenzi wa nyumba bora;

(ii) Maudhui na maelekezo ya sera hii yameweza kutafsiriwa na wadau mbali mbali ili yaendane na hali halisi ya eneo ambako inatekelezwa. Hii inazingatia ukweli kuwa jamii hazifanani na wala haziishi katika maeneo ambayo yana fursa na vikwazo vya maendeleo vinavyofanana. Matokeo ya tafsiri hizi yanaonekana katika tofauti ya mbinu shirikishi zinazotumika katika kila eneo;

(iii) Upo upungufu mkubwa kwa watumishi wa Maendeleo ya Jamii hususan katika ngazi za kata na vijiji. Pamoja na Sera kuhimiza kila kata na kijiji kiwe na Afisa Maendeleo ya Jamii, waliopo sasa hivi wanakidhi asilimia 40 tu ya mahitaji. Kwa sababu hiyo Wizara inaendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya Cheti na kuhimiza Halmashauri ziwaajiri ili kukidhi mahitaji.

(iv) Sera na mipango ya kisekta imezingatiwa vizuri na wananchi ambao wamewezeshwa kuimiliki na kuidumisha.

37. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na. 7 wa mwaka 2002, Maafisa Maendeleo ya Jamii Wasaidizi wanaajiriwa katika ngazi ya kata na vijiji. Ili kufanikisha utekelezaji wa Waraka huu Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Rungemba, Buhare na Missungwi viliendelea kufanyiwa ukarabati wa majengo na miundombinu ili kuviwezesha kutoa mafunzo ya taaluma ya Maendeleo

ya Jamii katika ngazi ya Cheti kwa waombaji wengi zaidi. Katika mwaka wa fedha 2004/2005 idadi ya wanachuo waliosajiliwa katika vyuo hivi ilikuwa 454. Kati yao wanawake walikuwa 315 sawa na aslimia 69.4 na wanaume 139 ambayo ni asilimia 30.6. Hili ni ongezeko la asilimia 65.6 ikilinganishwa na idadi ya wanachuo 298 waliosajiliwa mwaka 2003/2004.

38. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kutoa mafunzo ya taaluma katika ngazi ya Stashahada za juu, katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. Katika mwaka wa fedha 2004/2005. Jumla ya wanachuo 513 walipata mafunzo, kati yao wanawake ni 278 ambao ni sawa na asilimia 54.2 na wanaume ni 235 ikiwa ni sawa na asilimia 45.8. Idadi ya wanachuo imeongezeka kwa asilimia 31.5 ikilinganishwa na waliopatiwa mafunzo mwaka 2003/04. Vile vile Chuo kimeboreshwa kwa kufanya ukarabati wa mabweni, vyoo, mfumo wa maji na kimenunua vitanda, viti na magodoro.

39. Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako tukufu kwamba Wizara yangu, inaendelea kuratibu shughuli za Vikosi vya Ujenzi na programu ya Mafunzo ya Ufundi Vijijini ili visaidie jitihada za Serikali na za wananchi katika utekelezaji wa miradi ya kujitegemea inayohitaji ufundi. Nafurahi kuliarifu Bunge hili kuwa Wizara yangu kwa ushirikiano mzuri na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imewezesha Vikosi hivyo kubaki katika Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri ili kutoa nafasi kwa Wizara yangu kuwawezesha mafundi hawa. Katika kipindi cha 2004/05 jumla ya mafundi 40 kutoka Halmashauri 20 za Dodoma Mjini, Hai, Ifakara, Kilosa, Kondoa, Kongwa, Mahenge, Mbinga, Mjini, Morogoro Mjini, Morogoro vijijini, Moshi Mjini, Moshi Vijijini, Mpwapwa, Mwanga, Namtumbo, Rombo, Same, Songea Mjini, Songea Vijijini na Tunduru walipatiwa mafunzo kazini.

40. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa Mpango wa kutoa elimu, ujuzi na stadi mbali mbali za maendeleo katika vyuo 58 vya Maendeleo ya Wananchi. Jumla ya wananchi 24,658 wakiwemo wanawake 13,085 na wanaume 11,573 walipatiwa mafunzo, ikilinganishwa na wananchi 23,086 waliopatiwa mafunzo mwaka 2003/04. Hili ni ongezeko la asilimia 6.8. Mafunzo haya yalijumuisha ufugaji bora, ushonaji, useremala, ujasiriamali, hifadhi ya mazingira, mbinu za kudhibiti maambukizi ya virusi vya UKIMWI pamoja na nyinginezo za kuwawezesha wananchi kufanya kazi zao kwa ufanisi, kujiajiri na kujitegemea kama mkakati muhimu wa kuwawezesha kujipunguzia umaskini. Aidha, kutokana na ushirikiano mzuri na Halmashauri, vyuo hivi sasa vimeanza kuwa vitovu vya maendeleo katika maeneo yanayovizunguka. Nachukua nafasi hii kuzishukuru sana Bodi za Vyuo zinazoongozwa na Wakurugenzi wa Halmashauri, na kutambua mchango muhimu kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe. Kutokana na umakini wao, Bodi hizi zimeweza kubuni mbinu mbali mbali za kuviimarisha Vyuo hivi, ikiwa ni pamoja na kuboresha majengo, miundombinu na kuvipatia kazi mbali mbali za Halmashauri. Hatua hizi zimeviwezesha vyuo kujitegemea kwa kiwango kikubwa na kujiimarisha kimafunzo na kwa vitendo.

41. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/05 Wizara yangu ilianza kufanya ukarabati mkubwa wa majengo na miundombinu katika vyuo sita (6) vya Maendeleo ya Wananchi kwa utaratibu wa Chuo kimoja kila Kanda. Ukarabati huu ulifanyika katika Vyuo vya Gera (Kagera), Kisarawe (Pwani), Mbinga (Ruvuma), Msinga (Kilimanjaro), Ruaha (Iringa) na Urambo (Tabora). Aidha, vyuo vinane (8) vilifanyiwa ukarabati mdogo wa majengo na miundombinu. Vyuo hivyo ni Chala (Rukwa), Katumba (Mbeya), Kilosa (Morogoro), Kiwanda (Tanga), Mabughai (Tanga), Monduli (Arusha), Munguri (Dodoma) na Same

(Kilimanjaro). Jitihada hizi za Wizara yangu zinadhihirisha azma ya Serikali ya kuimarisha vyuo hivi kama chachu ya maendeleo. Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika maeneo ya vyuo hivi tayari wameanza kuona matokeo ya kazi zilizofanyika. Kwa kuwa majengo na miundombinu muhimu ya vyuo hivyo imekarabatiwa, hivi sasa wananchi wengi wamevutiwa na mazingira mazuri yaliyopo na wameanza kujiunga na vyuo hivyo kwa wingi.

42. Mheshimiwa Spika, ili kupunguza matatizo ya uvamizi wa maeneo ya vyuo na kuondoa migogoro ya ardhi inayovikabili, Wizara yangu ilipima maeneo ya vyuo kumi na moja (11) vya Bigwa (Morogoro), Handeni (Tanga), Kilwa Masoko (Lindi), Kiwanda (Tanga), Mabughai (Tanga), Malampaka (Shinyanga), Mbinga (Ruvuma), Munguri (Dodoma), Mwanva (Shinyanga), Same (Kilimanjaro) na Sengerema (Mwanza) ili viweze kupatiwa hati miliki. Mafanikio haya yametokana na ushirikiano mkubwa uliopo kati ya Wizara yangu na Halmashauri za Wilaya. Ni matumaini yangu kuwa vyuo hivi vitapata hati miliki hivi karibuni.

Idara ya Maendeleo ya Jinsia

43. Mheshimiwa Spika, takwimu za watu katika jamii nyingi zinaonyesha kuwa idadi ya wanawake ni kubwa kuliko ya wanaume, na ndio wenye jukumu kubwa la uzazi na kulea familia. Kutokana na ukweli huu, kuna kila haja kwa jamii kuwa na sera na mipango mahsusi ya kuwawezesha wanawake kutekeleza majukumu yao ya msingi katika nyanja mbali mbali za kiuchumi na kijamii ili kuhakikisha kuwa wanapata fursa za kimaendeleo na hali zao za maisha zinaboreshwa.

44. Mheshimiwa Spika, katika utayarishaji wa MKUKUTA, Wizara yangu iliteua Kamati maalumu ambayo ilipewa jukumu la kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanafafanuliwa wazi na kuingizwa katika

Mkakati huo. Vile vile Wizara iliendesha mkutano wa wanawake wadau mwezi Februari, 2005 Dar Es Salaam ambao pia ulihakikisha kuwa masuala ya jinsia yamezingatiwa katika MKUKUTA. Hata hivyo wadau hao walitoa angalizo kuwa haitoshi kuzingatia tu masuala ya jinsia katika MKUKUTA bali muhimu zaidi uwekwe katika utekelezaji wa maeneo hayo ili kuleta maendeleo ya wanawake na usawa wa jinsia unaokusudiwa.

45. Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa Dawati la Jinsia katika miundo ya Wizara, Mikoa na Halmashauri na Idara zinazojitegemea umeanza kuleta matokeo mazuri kwa kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanazingatiwa na kutekelezwa kama sehemu muhimu ya mchakato wa kuleta usawa wa jinsia na maendeleo. Ili kuboresha utendaji kazi wa Dawati la Jinsia, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilitoa mafunzo kwa baadhi ya Watendaji wa Dawati la Jinsia kuhusu namna ya kutathmini utekelezaji wa Ulingo wa Beijing na Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW). Matokeo ya mafunzo haya yaliwezesha Dawati hizi kutoa mchango mkubwa katika kuandaa taarifa ya miaka kumi ya utekelezaji wa Ulingo wa Beijing na taarifa ya tano ya nchi kuhusu CEDAW. Ili kupanua zaidi uelewa na ufahamu wa masuala hayo, Wizara iliwezesha ushiriki wa Watendaji wa Dawati la Jinsia katika mikutano ya kikanda na ya kimataifa. Kwa utaratibu huu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya, Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Ikulu zilishiriki katika kikao cha 49 cha Kamisheni ya Hali ya Wanawake kilichofanyika New York, Marekani mwezi Machi, 2005. Aidha, baadhi ya Wizara zimeunda kamati za masuala ya jinsia ndani ya Wizara zao. Kamati hizo zimewezesha watumishi wa Wizara kufahamu zaidi dhana ya usawa wa jinsia na kuweza kuandaa na kutekeleza

mipango inayozingatia jinsia. Huu ni mwitikio mzuri wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia.

46. Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu Maazimio mbali mbali ya kitaifa na kimataifa yanahimiza ushiriki wa wanawake katika vikao vya maamuzi ya kisiasa na vya utendaji katika ngazi zote za maamuzi. Kwa mfano, lengo la Umoja wa Afrika ni kufikia uwakilishi wa asilimia 50 na la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ni asilimia 30 hadi mwaka 2005. Mwaka huu, Bunge lako tukufu lilipitisha mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ambapo idadi ya viti maalum vya wanawake Bungeni inatarajiwa kufikia asilimia 30 mwishoni mwa mwaka huu. Kwa viti vya kuteuliwa na Rais uwiano utafikia kiwango cha Umoja wa Afrika cha asilimia 50 yaani, wanawake watano na wanaume watano. Mafanikio haya siyo madogo kwa kuwa yamedhihirisha wazi azma ya Serikali ya awamu ya Tatu chini ya uongozi wa Rais Benjamin William Mkapa, ya kuleta usawa wa jinsia katika vikao vya maamuzi. Aidha mwaka jana nilitoa rai kwa Wizara zote, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya kuhusu utekelezaji wa Azimio la SADC linalohusu Jinsia na Maendeleo ambalo pamoja na mambo mengine, linahimiza ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi usiwe chini ya asilimia 30. Rai hiyo ilizingatia kupitishwa kwa Sheria ya Utumishi wa Umma namba 8 ya mwaka 2002 iliyokasimia mamlaka ya ajira kwa Watendaji Wakuu na hivyo kutoa fursa kwa Kamati za Ajira kuzingatia uwiano mzuri wa jinsia katika kutoa ajira.

47. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 Wizara yangu iliahidi kufuatilia uanzishaji wa Chombo kitakachowaunganisha wanawake bila kujali itikadi za kisiasa na tofauti nyinginezo kama ilivyoainishwa katika Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Mwezi Oktoba, 2004

Baraza la Mawaziri lilielekeza kwamba uanzishaji wa Chombo usubiri matokeo ya shauri la Baraza la Wanawake Tanzania (BAWATA) lililopo mahakamani. Aidha agizo lilitolewa la kuhakikisha kuwa Wizara iimarishwe.

48. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeshirikiana na Asasi zisizo za Kiserikali (AZISE) na wanaharakati mbali mbali wanaoshughulikia masuala ya jinsia katika kuandaa taarifa ya tano ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake. Taarifa hii itawasilishwa katika Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia masuala ya Maendeleo ya Jinsia. Masuala makubwa yaliyojitokeza katika taarifa hiyo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa CEDAW umezingatia misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, maazimio ya kikanda, sera za jumla na za kisekta. Kutokana na hali hii imekuwa rahisi kwa wadau mbali mbali kuzingatia utekelezaji wa Mkataba huu katika mipango yao;

(ii) Jitihada zinazofanywa na wanaharakati wa masuala ya jinsia za kupiga vita ubaguzi dhidi ya wanawake zimeifanya jamii kuwa na uelewa mkubwa kuhusu masuala hayo na kushiriki kikamilifu katika kuleta usawa wa jinsia. Aidha jitihada hizo zimeonyesha haja ya kuwa na ushirikiano baina ya Serikali na wadau mbali mbali ili kuleta maendeleo stahimilivu yanayozingatia usawa wa jinsia katika jamii;

(iii) Sheria mbali mbali zilizotungwa na kudurusiwa katika kipindi cha miaka kumi ya Beijing zimezingatia utekelezaji wa Mkataba huu kwa misingi ya kuweka sheria zinazotetea usawa wa jinsia kwa kuondoa vipengele vinavyoashiria ubaguzi, unyanyasaji na ukatili dhidi ya wanawake;

(iv) Jitihada zimefanywa na Serikali, AZISE mbali mbali na Mabenki za kuwezesha wanawake kiuchumi ili waweze kuinua hali zao za maisha na kupunguza umaskini wa kipato unaowafanya washindwe kushiriki kikamilifu katika jitihada za kujenga uchumi;

(v) Wananchi kwa ujumla wamekuwa na mwamko na uelewa mkubwa kuhusu ubaguzi wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake na wamekuwa wakichukua hatua pale tabia za namna hiyo zinapojitokeza katika jamii;

(vi) Ukatili dhidi ya wanawake katika ngazi ya kaya hususan kupiga wanawake na mauaji ya wanawake wazee yamepungua;

(vii) Mila zenye madhara kama vile ukeketaji, kuoza watoto wa kike mapema na tabia nyingine zimeanza kupungua.

49. Mheshimiwa Spika, mwaka jana niliahidi kuandaa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Azimio na Ulingo wa Beijing kwa kipindi cha 1995 – 2005. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa taarifa hiyo iliandaliwa na kuzinduliwa rasmi na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya miaka kumi ya Azimio na Ulingo wa Beijing tarehe 2 Machi, 2005. Taarifa hiyo pamoja na kipeperushi ambacho kimeeleza kwa lugha ya Kiswahili utekelezaji huo, vimetawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge. Katika utekelezaji wa Azimio na Ulingo huu uliokuwa na maeneo 12, Tanzania ilitoa kipaumbele kwa maeneo manne makuu ambayo ni:- kuwawezesha wanawake kiuchumi na kuondoa umaskini; kuwapa wanawake haki na kuwaongezea uwezo kisheria; kuwapatia wanawake elimu, mafunzo na ajira; na kuwawezesha wanawake kushiriki katika ngazi za maamuzi. Katika maeneo yote haya kumekuwa na mafanikio makubwa na bado jitihada zinaendelea kufanywa na Wizara nyingine za kisekta.

50. Mheshimiwa Spika, katika eneo la kuwawezesha wanawake kujikwamua kiuchumi, Wizara yangu iliendelea na jitihada zake za kuratibu shughuli za utoaji wa mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (WDF). Aidha Wizara yangu ilitoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri 75 kuhusu mbinu na stadi za kuwahamasisha wanawake kujiunga na Vyama vya Kuweka na Kukopa (SACCOS). Vyama hivyo vinatarajiwa kwa kiasi kikubwa kuwawezesha wanawake kujiwekea akiba na kupata huduma za kifedha.

51. Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 Wizara yangu iliendelea kushirikiana na Asasi mbalimbali Zisizo za Serikali (AZISE) kuwawezesha wanawake kushiriki katika maonesho ya biashara ndani na nje ya nchi ili kuboresha bidhaa zao na kutafuta masoko. AZISE hizi ni pamoja na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote unaoendeshwa chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Mama Anna Mkapa na Shirikisho la Vyama Vya Wanawake Wafanyabiashara (FAWETA). Katika ushirikiano huu wanawake 130 waliwezeshwa kushiriki katika maonesho ya 28 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar Es Salaam mwaka 2004. Vile vile wanawake 254 wakiwakilisha vikundi 135 walishiriki maonesho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika mwezi Machi 2005 jijini Dar Es Salaam. Aidha wanawake 6 walishiriki katika maonesho ya kimataifa huko Botswana na mmoja aliweza kwenda Marekani kutafuta soko la bidhaa anazozalisha.

52. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mama Anna Mkapa, Mwenyekiti wa Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote, kwa kuwa mstari wa mbele katika kutekeleza Ulingo na Azimio la Beijing. Mheshimiwa Mama Mkapa kwa kipindi chote cha miaka kumi alipania kuhakikisha kuwa Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote unachangia kuwaimarisha wanawake

kiuchumi, kuongeza kipato na hivyo kukidhi mahitaji yao ya msingi. Ninamtakia heri katika maisha yake ya baadaye na ninaahidi kuwa Wizara yangu itaendelea kushirikiana naye kikamilifu katika mipango yote yenye lengo la kuleta maendeleo ya wanawake na usawa wa jinsia.

Maendeleo ya Mtoto

53. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kuhakikisha kuwepo kwa mazingira mazuri yanayowafanya watoto kukua na kupata ustawi kulingana na malezi bora ya familia na jamii. Katika kipindi cha mwaka 2004/05 Wizara yangu iliendelea na jitihada za kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto inayotekelezwa na wadau mbali mbali. Vile vile Wizara imeendelea kuelimisha jamii kupitia kaulimbiu mbali mbali za maadhimisho kama vile siku ya Mtoto wa Afrika, Siku ya Familia Duniani, Siku ya Unyonyeshaji Duniani, Siku ya UKIMWI Duniani, Siku ya Kudhibiti Ukeketaji Duniani na Siku ya kukomesha utumikishwaji wa watoto Duniani.

54. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kama Mratibu wa Mtandao wa watoto chini ya miaka minane (Tanzania Early Childhood Development Network), kwa kushirikiana na wadau wengine, imefanya uchunguzi wa awali wa hali halisi ya watoto. Uchunguzi huu unaonyesha kuwa watoto walio katika umri wa awali wanakabiliwa na matatizo mengi ambayo ni pamoja na maambukizi ya UKIMWI, kubakwa, kutupwa, kutelekezwa na kukosa malezi mazuri na lishe bora. Kutokana na kutambua tatizo hili Tanzania iliungana na nchi nyingine nne za Afrika kuandaa mpango maalum wa kuwasaidia watoto walio chini ya umri wa miaka minane walioathiriwa au kuathirika na virusi vya UKIMWI na UKIMWI. Nchi hizo ni Ghana, Malawi, Namibia na Zambia. Aidha, Tanzania ilihudhuria mkutano wa tatu wa Kimataifa Barani Afrika kuhusu Maendeleo na Makuzi ya Awali ya Utotoni uliofanyika Ghana mwezi Juni, 2005. Katika

mkutano yote hiyo iliazimiwa kuwa masuala ya maendeleo na makuzi ya awali ya utotoni yapewe kipaumbele katika maeneo yanayolenga kuimarisha maisha ya watoto, hususani wale walio katika mazingira magumu.

55. Mheshimiwa Spika, utumikishwaji wa watoto bado unaendelea kuwa tatizo la kijamii. Ili kulitafutia ufumbuzi tatizo hili, Wizara yangu inashirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) katika kuratibu utekelezaji wa Programu ya Taifa ya muda maalum ya kukomesha Utumikishwaji wa Watoto katika kazi za hatari. Aidha katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Wizara yangu ilikamilisha mradi wa kuingiza masuala haya katika mitaala ya Mafunzo ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Lengo ni kuhakikisha kuwa wahitimu wa vyuo hivi wanakuwa na mbinu na stadi za kuihamasisha jamii kupambana na utumikishwaji wa watoto.

56. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mkataba wa Haki za Mtoto unaendelea kwa kushirikiana na wadau zikiwemo sekta za Serikali na AZISE mbali mbali kama KULEANA, KIWOHEDE, Kituo cha Watoto Wadogo, Plan (T) na Save the Children, zinazoshughulikia masuala ya watoto. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba taarifa ya utekelezaji ya Tanzania imetayarishwa na kupelekwa kwenye Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Mtoto.

57. Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2004/05 nililiarifu Bunge lako tukufu kwamba ziko mila na desturi zinazoleta madhara kwa jamii na hasa wanawake na watoto ambazo zinahitaji kutokomezwa, mojawapo ikiwa ni ya ukeketaji. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa kupitia mikutano ya Mtandao wa Kutokomeza Ukeketaji, katika Kanda ya Afrika Mashariki Tawi la Tanzania na wanaharakati mbalimbali, Wizara imeboresha mbinu za kuondokana na

mila hii zikiwemo kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya ukeketaji na kuwapa ngariba mafunzo ya kuwawezesha kufanya shughuli nyingine za kiuchumi.

58. Mheshimiwa Spika, matokeo ya jitihada hizi ni kupungua kwa kiwango cha ukeketaji wa wanawake na watoto wa kike hapa nchini. Utafiti uliofanywa mwaka 2003/04 na Mtandao wa Kupambana na Ukeketaji (Anti-Female Genital Mutilation - AFNET) unaonyesha kuwa katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Manyara, Morogoro na Singida, ngariba 2026 walitangaza hadharani kuacha kazi ya ukeketaji. Wizara yangu inafuatilia kwa karibu matokeo haya ili yawe ya kudumu. Wizara yangu kama Mwenyekiti wa Mtandao wa Kudhibiti Ukeketaji Kanda ya Afrika Mashariki Tawi la Tanzania inaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji hapa nchini kwa kushirikiana na asasi zisizo za serikali. Nachukua nafasi hii kuzipongeza asasi hizo kwa jitihada wanazozifanya.

Utawala na Utumishi

59. Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Utumishi ina jukumu la kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma mahala pa kazi unaimarishwa. Jukumu hili linatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2002, Sheria ya Fedha Namba 6 ya mwaka 2001 na Sheria ya Ununuzi Namba 4 ya mwaka 2001. Kupitia sheria hizi mwaka 2004/05 Kamati ya Ajira ya Wizara iliweza kuajiri watumishi 72, kutangaza tenda 3 na kusimamia kazi na manunuzi mbali mbali. Aidha, Wizara ilipata shs. 164,000,000 za ununuzi wa vifaa vya ofisi kutoka Mfuko wa Kuongeza Ufanisi unaosimamiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

60. Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa idadi ya kutosha ya watumishi wenye sifa na uwezo unaotakiwa ni suala muhimu katika kufikia malengo ya Mpango Mkakati wa Wizara (Strategic Plan). Katika kipindi hicho watumishi 56 wa Wizara yangu walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa lengo la kukidhi mahitaji ya kazi na matakwa ya miundo yao ya utumishi.

61. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 iliendelea kuwaelimisha watumishi wake juu ya mapambano dhidi ya rushwa kupitia vikao mbali mbali vya kazi. Wananchi nao wameelimishwa kupitia maadhimisho mbali mbali ya kitaifa yanayoratibiwa na Wizara hii. Aidha, mpango wa utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa wa mwaka 2002 ni miongoni mwa maeneo yaliyo katika MKUKUTA ambayo utekelezaji wake unaanza katika mwaka wa fedha 2005/2006.

62. Mheshimiwa Spika, katika kupambana na UKIMWI mahali pa kazi, Wizara iliendelea kutoa elimu kuhusiana na masuala ya UKIMWI. Jumla ya watumishi 48 walipatiwa mafunzo hayo katika warsha iliyofanyika Mkoani Morogoro tarehe 17 hadi 21 Februari, 2005, na watumishi 250 katika warsha iliyofanyika Iringa kuanzia tarehe 30 Mei, 2005 hadi 03 Juni, 2005.

63. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara yangu iliendelea kutekeleza programu ya kuboresha Utumishi wa Umma kwa kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma za usafi wa ofisi na mazingira na ulinzi na usalama kwenye ofisi za Makao Makuu ya Wizara.

64. Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2004/2005, niliahidi kuwa Wizara ingeimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Umma kwa kununua vifaa mbali mbali pamoja

na kuongeza wataalam. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba kupitia Mfuko wa Kuongeza Ufanisi (Performance Improvement Fund), Kitengo kimetengewa fedha zitakazotumika kununulia vifaa vya kisasa. Lengo ni kuhakikisha kuwa majukumu ya Kitengo hiki yanatekelezwa ikiwa ni pamoja na utoaji wa habari zinazohusu utekelezaji wa Sera za Wizara kwa umma. Aidha watumishi wa Kitengo hiki wamekwisha ajiriwa.

Sera na Mipango

65. Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako tukufu kwamba Wizara yangu iliandaa mpango wa mwaka mmoja (Interim Plan) ili kutoa nafasi ya kukamilisha taratibu za kupata ufadhili wa pamoja wa wahisani. Taratibu hizi zimekamilika na utayarishaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitatu umeanza.

66. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanza maandalizi ya uwekaji wa kumbukumbu zinazohusu wanawake katika kompyuta (Women's Database). Hatua zifuatazo zimefikiwa katika kutekeleza mradi huu:-

(i) Fomu za kukusanya kumbukumbu zinazohusu wanawake zimeandaliwa na kujaribiwa kwa baadhi ya watumishi wa Wizara;

(ii) Mfumo wa kompyuta wa kuhifadhi kumbukumbu hizo umebuniwa na kujaribiwa kwa mafanikio;

(iii) Fomu za kukusanya kumbukumbu hizo zimeanza kusambazwa katika taasisi mbali mbali ili waajiriwa wanawake wazijaze na kuzirudisha Wizarani.

Kumbukumbu hizo zitaisaidia Serikali kufahamu wasifu wa wanawake waliopo katika maeneo mbali mbali ya utumishi na kuzifanyia kazi, ikiwa

ni pamoja na kupendekeza majina ya wanawake wenye sifa za kushika nafasi za uongozi ndani na nje ya nchi.

67. Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo wa ufuatiliaji na tathmini unaozingatia jinsia (Computerized Gender Sensitive Monitoring and Evaluation system), takwimu kutoka kwenye Wizara, Idara za Serikali, Halmashauri za Miji, Manispaa na wilaya zimeanza kukusanywa. Kazi hii imeshaanza kufanyika katika Wizara yangu, na inaendelea kufanyika katika Wizara na Taasisi nyingine.

V. MIPANGO NA MALENGO YA MWAKA 2005/06

68. Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini hiyo, sasa naomba kutoa taarifa ya mipango na malengo ya Wizara yangu kwa mwaka 2005/2006.

69. Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) umeleta mabadiliko makubwa katika mgawanyo wa majukumu na kufanya kila sekta ihusike moja kwa moja katika utekelezaji wa malengo makuu ya MKUKUTA yafuatayo:-

(i) Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato;

(ii) Kuimarisha hali za maisha;

(iii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

Malengo haya yamenyumbuliwa kwa kuzingatia mchango wa kila sekta ambapo Wizara yangu ina jukumu la kutekeleza malengo 34 yanayohusu masuala ya maendeleo ya jamii, maendeleo ya wanawake, jinsia na watoto.

Maendeleo ya Jamii

70. Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kuwa bila ushiriki wa jamii katika kutekeleza MKUKUTA malengo yaliyowekwa hayataweza kufikiwa na kudumishwa. Kutokana na ukweli huu, Wizara yangu itaendelea na jukumu lake la kuhakikisha kuwa wananchi wanahamasishwa ili wajitokeze kushiriki kikamilifu katika kutekeleza MKUKUTA. Ili kufikia lengo hili Wizara itaendelea kutoa wataalam wa maendeleo ya jamii, kuhamasisha jamii kushiriki katika kutekeleza MKUKUTA. Aidha, kwa Chuo cha Tengeru, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira kwa kujenga ukumbi wa mihadhara, kuweka intaneti, huduma ya usafiri na kuunda Bodi ya Uendeshaji itakayosimamia Chuo.

71. Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya wananchi, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo ya ndani na nje katika vyuo 58 vya maendeleo ya wananchi ili kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi. Jumla ya wananchi 25,000 wanatarajiwa kupata mafunzo mwaka huu. Mafunzo na stadi mbali mbali zitakazotolewa Vyuoni na nje ya Vyuo zitawawezesha wananchi kujitegemea na kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na tija zaidi. Mafunzo hayo yatatolewa kwa kuzingatia maeneo yafuatayo ya MKUKUTA:-

(i) Kuwezesha mafunzo ya stadi za maisha na ujasiriamali kwa ajili ya wananchi vijijini hususan wanawake na vijana;

(ii) Kuongeza mafunzo ya stadi za kisomo chenye manufaa kwa wanawake na wanaume watu wazima ili kuwawezesha kufanya shughuli mpya kwa kadri umri unavyoongezeka;

(iii) Kuelimisha jamii kuhusu haki za msingi za mtoto, pamoja na mapambano dhidi ya ajira mbaya, kuandaa na kutekeleza mipango inayolenga kuondoa ajira kwa watoto;

(iv) Kuinua matumizi ya habari, mawasiliano na teknolojia katika Taasisi za Serikali na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(v) Kuweka misingi imara inayolenga watu wenye ulemavu, watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, wagonjwa, wazee pamoja na watoto, kupata huduma za jamii, misaada, mikopo na misamaha ya uchangiaji gharama mbali mbali vyuoni na katika sekta mbali mbali zinazotoa huduma;

(vi) Kuwawezesha watoto wa kike wanaokatisha masomo kutokana na kupata mimba kumaliza masomo yao au kuwapatia stadi za ufundi;

(vii) Kusaidia kaya zilizoathiriwa na UKIMWI ambazo zinaongozwa na vijana wa kike, watoto na wazee kwa kuwawezesha kupata huduma za kijamii, zikiwemo misamaha katika uchangiaji gharama za huduma mbali mbali, utunzaji wa wagonjwa nyumbani na utoaji wa mafunzo ya stadi.

72. Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya maeneo haya, Wizara yangu inakusudia kukamilisha ukarabati mkubwa wa majengo na miundombinu ulioanza mwaka jana. Aidha, Wizara inakusudia kuweka mitambo ya umeme inayotumia nguvu ya jua kwenye vyuo vinane (8) ambavyo havijafikiwa na umeme wa gridi. Vile vile, Wizara itawezesha upimaji wa maeneo ya Vyuo vinane (8) vya Maendeleo ya Wananchi ili kuvipatia hati miliki.

73. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/06, Wizara yangu inakusudia kufuatilia hali ya Majumba ya Maendeleo (Community Centres) yaliyokuwa yanasimamiwa na Mabibi na Mabwana Maendeleo

yaliyojengwa zamani, kwa madhumuni ya kuyafufua ili kuwawezesha wananchi kupata habari kuhusu maendeleo kubadilishana uzoefu kutoka ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara inakusudia kuyapatia majumba hayo vifaa na nyenzo muhimu kama majarida, luninga, kanda na kompyuta zitakazowawezesha wananchi kupata na kupashana habari za maendeleo.

74. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa ushiriki wa jamii katika jitihada mbali mbali za hifadhi ya mazingira. Kwa kuanzia, Wizara yangu itashirikiana na mikoa ya Iringa na Mbeya kuhamasisha wananchi kushiriki katika kampeni dhidi ya uharibifu wa mazingira katika maeneo ambayo ni vyanzo vya mto Ruaha. Maeneo haya yamepewa kipaumbele kwa kuwa sehemu kubwa ya umeme wa gridi nchini huzalishwa katika mabwawa ya Kidatu na Mtera ambayo yote yamejengwa katika mto huo.

75. Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna ongezeko la wasichana na wavulana wanaoishi katika mazingira magumu, wengi wao wakiwa wameshindwa kumaliza elimu ya msingi au ya sekondari. Katika kuchangia kupunguza ukubwa wa tatizo hili, Wizara yangu itawahamasisha na kuwawezesha wanafunzi katika mikoa saba waliokatisha masomo kushiriki katika shughuli zitakazowaongezea kipato. Aidha, Wizara itatoa fursa maalumu za mafunzo ya stadi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa watoto yatima na walio katika mazingira magumu na hatimaye kuwapatia vifaa vitakavyowawezesha kujiajiri baada ya kufuzu mafunzo hayo. Hii itakuwa hatua maalumu (affirmative action) kwa walengwa hawa.

76. Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa inapata majanga mbali mbali kama vile mafuriko, njaa na magonjwa ya milipuko. Wananchi wengi wanashindwa kukabiliana nayo ipasavyo kutokana na ukosefu wa

mbinu shirikishi za kuwawezesha kumudu hali inayotokana na maafa hayo. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara yangu itatoa elimu kwa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri kuhusu mbinu shirikishi za kukabiliana na maafa. Mbinu hizo zitawawezesha wananchi kushiriki katika kukabiliana na maafa pindi yanapotokea na kumudu matokeo ya maafa hayo.

77. Mheshimiwa Spika, UKIMWI umesababisha familia nyingi kuongozwa na wanawake, vijana, watoto au wazee wenye uwezo mdogo wa kujitunza wao wenyewe na familia zao. Ili kuchangia ufumbuzi wa tatizo hili, Wizara yangu itatoa mafunzo kwa wataalamu wa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ili waweze kuandaa mipango ya kupambana na UKIMWI kwa kushirikiana na jamii katika ngazi ya kijiji. Aidha, wataalam watatumika katika kubaini wajibu na majukumu ya wadau mbali mbali katika kutekeleza mipango hiyo.

78. Mheshimiwa Spika, kwa kupitia MKUKUTA, Wizara yangu itawawezesha kinyenzo baadhi ya Maafisa wa Maendeleo ya Jamii kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Kwa mwaka 2005/06, Wizara yangu itaanza kwa kuwapatia pikipiki moja moja Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri 20. Hali kadhalika Wizara itawapa mafunzo ya kuongeza elimu ili waweze kukidhi matakwa ya miundo yao mipya ya utumishi kama sheria ya Utumishi wa Umma inavyoelekeza. Aidha, uwezo wa wakufunzi wa vyuo utaboreshwa kwa kuwapa mafunzo kazini, mafunzo ya kompyuta na ya menejimenti.

Maendeleo ya Wanawake na Jinsia

79. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza MKUKUTA, Wizara yangu itaandaa mwongozo utakaohakikisha kuwa maeneo yanayohusu jinsia yanatekelezwa kikamilifu. Mafunzo ya matumizi ya mwongozo huo

yatatolewa kwa watendaji mia moja (100) wa Dawati la jinsia, katika ngazi za Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri na sekta nyingine. Aidha, mwongozo huo utakuwa ni sehemu ya mfumo mzima wa kitaifa wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa MKUKUTA.

80. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza jitihada za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake Wizara yangu katika mwaka 2005/2006 itachapisha nakala 2,000 za Mpango wa Taifa wa kuondoa aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na kuzisambaza. Vile vile, Maafisa Maendeleo ya Jamii na Wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na vya Maendeleo ya Jamii wataelimishwa kuhusu mpango huu ili waweze kuanza kutoa elimu kuhusu athari za ukatili dhidi ya wanawake na jinsi ya kuutokomeza kwa jamii inayozunguka Vyuo hivyo. Pamoja na hatua hii, Wizara itaendesha mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii 114 ili wapate mbinu na stadi za kutoa ushauri nasaha kwa waliodhurika na vitendo vya ukatili. Aidha, jitihada zitafanywa kuwaelekeza na kuwawezesha wanawake kupata msaada wa kisheria pale inapobidi kufanya hivyo.

81. Mheshimiwa Spika, sheria kadhaa hapa nchini zimerekebishwa au kupitishwa kwa lengo la kuleta haki na usawa wa jinsia. Sheria hizi ni pamoja na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998, Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999. Kwa kuwa wananchi wengi hawayafahamu maudhui ya sheria hizi, Wizara yangu itaandaa majarida na vipeperushi kwa lugha nyepesi kwa ajili ya kuelimisha jamii kuhusu mabadiliko hayo yenye lengo la kutoa haki kwa wanawake.

82. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuiwakilisha nchi katika mikutano ya kikanda na kimataifa inayohusu maendeleo ya

wanawake na jinsia, kama ile ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), Kamisheni ya Hali ya Wanawake (CSW), Nchi za Maziwa Makuu, Kamisheni ya Uchumi ya Afrika (ECA) na Jumuiya ya Madola (Commonwealth) kwa madhumuni ya kuweka mikakati ya pamoja na kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa maazimio mbali mbali.

83. Mheshimiwa Spika, katika kupunguza umaskini wa kipato na kuwezesha Wanawake kiuchumi, na kama ilivyoelekezwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu utekelezaji wa mpango wa kupanua huduma za fedha vijijini, Wizara yangu itaendelea kuwezesha wanawake kujiunga na Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa (SACCOS) na vile visivyo vya Ushirika (SACAS). Aidha, mafunzo ya mbinu na stadi za kuhamasisha wanawake yatatolewa kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri. Pamoja na hatua hizi, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Ndogo Ndogo Tanzania (MKURABITA) unategemewa kuwawezesha wanawake kutumia mali zilizorasimishwa kama dhamana ya mikopo kutoka Benki mbali mbali.

84. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa mwaka 2005/2006 itaendelea kuratibu, kusimamia na kufuatilia uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya jamii ambao katika semina ya mikakati ya kuboresha Mfuko huu waliweza kutoa mapendekezo ya kuuimarisha. Mapendekezo yao yatazingatiwa. Ni lengo la Wizara yangu kufanya tathmini ya kina kuhusu uendeshaji wa Mfuko huu, hasa kwa kutia maanani tatizo kubwa la marejesho. Tathmini hiyo italenga kutumia Mfuko huu kuziimarisha SACCOS na SACAS na hatimaye kuwezesha kuundwa kwa Benki Kata.

85. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha jitihada zilizopo za kuwawezesha wanawake wajasiriamali kupata masoko ya ndani na nje, Wizara yangu katika mwaka 2005/2006 itaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na mashirika mengine kuwawezesha wanawake kushiriki katika maonyesho ya kimataifa ya ndani na ya nje ya nchi ili kupanua wigo wa masoko ya bidhaa zao. Msisitizo utakuwa katika kuboresha na kunakshi bidhaa zao. Aidha, Wizara yangu itaendelea na jukumu la kuratibu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa madhumuni ya kuongeza ufahamu wa jamii kuhusu umuhimu wa usawa wa jinsia katika kuleta maendeleo stahimilivu.

86. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalo jukumu la kutathmini utekelezaji wa programu na miradi mbali mbali ya maendeleo ili kuona ni kwa jinsi gani inazingatia masuala ya jinsia. Ufuatiliaji na ukusanyaji wa takwimu za jinsia utafanywa kwa kutumia miongozo iliyotolewa na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia; Mkakati wa Maendeleo ya Jinsia na MKUKUTA. Katika mwaka wa fedha 2005/06, Wizara itaanza kukusanya takwimu kutoka sekta sita za kijamii kwa kutumia maafisa wa Dawati la Jinsia. Matokeo ya zoezi hili yatawekwa katika mfumo wa Wizara unaochanganua takwimu kijinsia (Gender Disagregated Data).

87. Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa na TACAIDS umeonyesha kuwa kasi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa Watanzania ni asilimia 7. Hata hivyo wanawake wako katika kasi kubwa zaidi ya kuambukizwa ya asilimia 7.7, ikilinganishwa na wanaume ambao wapo kwenye kasi ya asilimia 6.3. Msemo kuwa UKIMWI umechukua sura ya mwanamke unatokana na takwimu hizi, na jukumu kubwa walilonalo la kulea wagonjwa na yatima. Kwa kupitia MKUKUTA, Wizara yangu itashirikiana na TACAIDS kuihamasisha jamii hususan wanaume ili

washiriki kikamilifu katika kuchukua hatua za pamoja za kushughulikia masuala ya kijinsia yanayosababisha kasi ya maambukizi kuongezeka kwa wanawake na wasichana. Aidha Wizara yangu itabainisha mahitaji ya kijamii na kuwaelekeza kwenda kwenye asasi mbali mbali zinazotoa misaada ikiwa ni pamoja na kuvitumia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kupata mafunzo kuhusu mbinu na stadi.

Maendeleo ya Mtoto

88. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kusambaza Sera ya Maendeleo ya Mtoto hasa kwa watoto ambao ni wadau wakubwa, ili waielewe Sera hiyo. Katika kipindi cha mwaka 2005/06, Wizara yangu itakamilisha zoezi la kuiweka Sera hiyo katika lugha nyepesi kabla ya kuisambaza kwa wadau mbali mbali kwa kuwa jukumu la kulea watoto ni letu sote.

89. Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2004/05, nililieleza Bunge lako tukufu kuhusu umuhimu wa kuelimisha jamii ili kuongeza uelewa wao wa Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia (Population and Family Life Education - POFLEP). Kwa kuzingatia hali hiyo, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka huu, itadurusu mtaala wa mafunzo katika ngazi ya jamii na itaendelea na hatua ya kutoa elimu kuhusu Elimu ya Idadi ya Watu na Maisha ya Familia.

90. Mheshimiwa Spika, mojawapo ya majukumu yaliyotolewa kwa Wizara yangu kupitia MKUKUTA, ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa makubaliano yaliyomo katika mikataba ya kimataifa kuhusu haki na ustawi wa mtoto. Katika kipindi cha mwaka 2005/06, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau, inatarajia kutayarisha taarifa ya kwanza ya utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto na

kuiwasilisha Umoja wa Afrika Addis Ababa, Ethiopia. Aidha Wizara yangu kwa kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi itaelimisha jamii inayozunguka Vyuo hivyo kuhusu haki za msingi za mtoto, zikiwemo haki ya kuendelezwa, kulindwa na kutotumikishwa katika kazi za hatari.

91. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/06, Wizara yangu itatoa elimu ya malezi na maendeleo ya awali ya mtoto kwa jamii zinazozunguka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Ilula, Mamtukuna, Nzovwe na Ulembwe. Aidha, Wizara yangu itaviwezesha Vyuo hivyo kuendelea kutoa mafunzo ya majaribio (pilot) kwa ajili ya kuratibu utekelezaji wa programu inayohusu wasichana waliokatisha masomo yao, kama wale waliojifungua katika umri mdogo. Eneo jingine ni kufanya utafiti ili kuweza kushughulikia matatizo ya watoto wanaozaliwa magerezani au wanaolazimika kuandamana na mama zao magerezani.

92. Mheshimiwa Spika, mwaka huu, Wizara yangu itaziwezesha jamii zilizoathirika zaidi na ongezeko la watoto yatima kutayarisha mipango shirikishi jamii itakayobaini maeneo mbali mbali ya kufanyiwa kazi, na wajibu wa makundi yanayowasaidia watoto yatima na walio katika mazingira magumu. Mikoa itakayohusika na zoezi hili kwa mwaka huu ni Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Ruvuma na Singida. Mipango hii itaziwezesha jamii kufahamu fursa zilizopo katika jamii za kuwawezesha kupambana na tatizo hili. Aidha nafasi ya wadau mbali mbali na Serikali katika kutekeleza mipango hii zitafahamika.

93. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/06, Wizara yangu itatayarisha programu ya kupunguza utumikishwaji wa watoto katika kazi za hatari. Hivyo Wizara yangu inakusudia kufanya utafiti wa awali kuhusu usafirishaji wa watoto ndani na nje ya nchi (human trafficking). Vile vile, Wizara itaendesha zoezi la kuelimisha jamii dhidi ya

utumikishwaji wa watoto kwa kutumia vyombo vya habari kama radio, magazeti na televisheni kwa kushirikiana na wanaharakati katika mikoa ya Singida na Iringa.

94. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/06 Wizara yangu itatekeleza lengo la MKUKUTA la kutayarisha mpango wa kitaifa wa elimu ya malezi ya watoto wadogo chini ya umri wa miaka mitano kwa kushirikiana na wadau mbali mbali. Madhumuni ya hatua hii ni kuimarisha malezi na makuzi ya watoto wachanga na wadogo nchini. Aidha Wizara yangu itakusanya na kusambaza zana za ushawishi jamii kuhusu ubora wa maziwa ya mama na hatari za ulikizaji pale mtoto anapoacha kunyonya ziwa la mama.

95. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/06 Wizara yangu itabaini matatizo yanayozikabili kaya zinazoongozwa na watoto yatima na walioathirika kwa UKIMWI katika maeneo yanayozunguka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Matokeo ya utafiti huo yataziwezesha jamii kuandaa mipango shirikishi jamii ya kuwasaidia watoto hawa.

Utawala na Utumishi

96. Mheshimiwa Spika, ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu itaendelea na majukumu ya kuajiri, kuwezesha utendaji kazi katika idara mbali mbali, kutoa mafunzo ya kimenejimenti na taaluma, kuendeleza utawala bora, kupambana na rushwa pamoja na kukabiliana na janga la UKIMWI mahala pa kazi.

97. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu itazindua na kuanza rasmi utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Mkataba huu unaainisha viwango vya huduma ambavyo

umma unavitarajia na umeweka miundo ya ufuatiliaji na utatuzi wa matatizo pale yanapojitokeza. Aidha, watumishi wote wa Wizara yangu watakamilisha zoezi la kutathmini Mpango Mkakati wa Wizara.

98. Mheshimiwa Spika, Serikali iliwaagiza waajiri kuwaendeleza watumishi wote ambao hawana sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo yao ya utumishi ili kuhakikisha wanapata sifa hizo katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai, 2004. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara itaendelea kuwaimarisha watumishi ili wafanye kazi zao kwa ustadi na maarifa zaidi.

99. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika mapitio ya utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara kwa mwaka 2004/2005, Wizara yangu inakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi ikilinganishwa na wingi wa majukumu yanayopaswa kutekelezwa hasa katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu inatarajia kuajiri watumishi wapya 50 kama tulivyoidhinishiwa.

100. Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa mwongozo kuhusu masuala ya ajira katika Utumishi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu itaboresha utendaji wa Kamati ya Ajira ya Wizara ili iweze kuutumia kikamilifu mwongozo wa ajira unaosisitiza ushindani na kuhakikisha kuwa wote wanaoajiriwa katika Utumishi wa Umma wana taaluma, ujuzi na sifa zinazotakiwa.

101. Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya rushwa yamepewa msukumo mpya kwa kuingizwa kwenye maeneo muhimu yanayotarajiwa kutekelezwa chini ya MKUKUTA. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa

watumishi na kusambaza miongozo ya maadili, sheria, kanuni na taratibu zinazohusu mapambano dhidi ya rushwa sambamba na utoaji mafunzo kwa watumishi wa Wizara.

102. Mheshimiwa Spika, udhibiti wa UKIMWI sehemu za kazi una lengo la kuhakikisha kuwa watumishi wana afya njema inayowawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kutimiza lengo hili Wizara yangu imeunda Kamati ambapo katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara itawawezesha wafanyakazi kubaini masuala yanayochochea maambukizi ya UKIMWI. Utambuzi huu utasaidia kuwaelimisha wafanyakazi na kuwatia hamasa wabadili tabia. Kuhusu watumishi walioathirika, Wizara itaendelea kutoa baadhi ya misaada kama vile dawa na ushauri nasaha.

103. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji kati yake, Wizara na taasisi mbali mbali pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali ambao ni wadau wetu kwa kupitia Mkutano Mkuu wa Mwaka. Vile vile tutaendelea na mikutano miwili kwa mwaka ya Mashirikiano kati ya Wizara yangu na Wizara ya Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Zanzibar. Aidha, mahusiano kati ya Menejimenti na watumishi yataimarishwa kupitia Baraza la wafanyakazi litakalokutana mara mbili kwa mwaka.

104. Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Wizara yangu kuwezesha taasisi na umma kwa ujumla kupata habari kuhusu masuala mbali mbali ya maendeleo ya jamii, jinsia na watoto kama yalivyofafanuliwa katika Sera za Wizara. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara yangu itaendelea kukitumia Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ya Umma kufanikisha azma hii. Aidha, Kituo cha Habari kuhusu wanawake kitakuwa sehemu ya kitengo hiki baada ya ufadhili wa AIDOS (Asasi isiyo ya kiserikali) iliyokuwa inaendesha kituo hiki kukamilisha mkataba

na kukikabidhi Wizarani. Nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali ya Italia na uongozi wa AIDOS kwa kukifadhili na kukiendesha kituo hiki takriban kwa muda wa miaka kumi.

105. Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika Mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Majukumu ya Wizara kwa mwaka 2004/2005, Wizara imeanza utekelezaji wa tathmini ya utendaji kazi kwa mwaka. Utaratibu huu wa uwazi unakuwa mbadala wa taratibu nyingine zilizokuwa zikitumika katika utumishi wa umma. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara itaendelea na utaratibu huu kwa kuandaa na kuwekeana mikataba ya kazi na watumishi wake wote kwa lengo la kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma. Aidha, Wizara yangu itaendelea na utekelezaji wa programu ya kuboresha Utumishi wa Umma kwa kuishirikisha sekta binafsi katika usafi wa ofisi na mazingira yake pamoja na ulinzi wa mali za Serikali na kuendelea kuibua maeneo mengine ambayo sekta binafsi zinaweza kutoa huduma Wizarani.

Sera na Mipango

106. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itafanya ukaguzi wa utekelezaji wa bajeti yake, ikiwa ni pamoja na ukaguzi katika vyuo vya Maendeleo ya Jamii na vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na shughuli mbali mbali zinazotekelezwa chini ya MKUKUTA ili kubaini maeneo yenye upungufu na kuurekebisha. Aidha Wizara itafuatilia utekelezaji wa sera zake katika Asasi zisizo za kiserikali kwa ajili ya kutathmini mafanikio ya sera hizo na kuimarisha uhusiano na Asasi hizo.

107. Mheshimiwa Spika, Wizara itafanya utafiti kuona kama Sera zake mbali mbali zinawafikia wana-jamii, wanazielewa na kama zimeweza kubadilisha hali na mienendo ya maisha yao. Aidha Wizara itaangalia ni

kwa kiwango gani jamii inaelewa Maazimio ya Beijing na Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW).

108. Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililieleza Bunge lako tukufu kuwa Wizara yangu iliandaa mpango wa mwaka mmoja (Interim Plan) ili kutoa nafasi mpango wa miaka mitatu kukamilishwa. Kwa kushirikiana na mtaalam, mpango huu wa mwaka mmoja utaendelea kutekelezwa wakati mpango wa miaka mitatu unakamilishwa.

VI: MWISHO

109. Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la Wizara yangu ni kutayarisha sera na miongozo mbali mbali yenye mwelekeo wa kuzihamasisha jamii kujiletea maendeleo kwa kuziwezesha kushiriki katika utekelezaji wa mikakati mbali mbali ya kukuza uchumi na hatimaye kupunguza umaskini. Majukumu haya ni mtambuka. Hivyo basi, utekelezaji wa malengo na mipango ya Wizara ya mwaka 2005/2006 bado utahitaji ushirikiano mkubwa zaidi wa wadau mbali mbali hasa Mikoa na Halmashauri. Tutaendelea kushirikiana na wadau hawa na vile vile kuziwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika maendeleo yao wenyewe na taifa zima kwa ujumla.

Pongezi na Shukrani

110. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Shamim Parkar Khan (Mb.), Naibu Waziri, kwa ushirikiano na ushauri wake mkubwa alionipa katika kipindi chote cha uongozi wangu ndani ya Wizara hii. Vile vile napenda kumshukuru Bibi Hilda Ausi Gondwe, Katibu Mkuu, kwa ushirikiano na msaada anaonipa katika kuimarisha misingi na mwelekeo mzuri wa Wizara yangu.

Vile vile, napenda kuwashukuru Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara yangu katika ngazi zote na katika taasisi zetu zote kwa ushirikiano wao, hususan katika kutekeleza majukumu ya Wizara ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako tukufu. Ushirikiano wa wote hawa na michango yao imefanya uongozi wangu kuwa mwepesi na kutuwezesha kulitumikia taifa letu kikamilifu.

111. Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kutumia nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa washirika wa ndani ambao wameshirikiana nasi kwa namna moja au nyingine katika kutekeleza majukumu yetu. Washirika hao ni pamoja na; Mtandao wa Kupambana na Ukeketaji (AFNET), Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*), Shirika la Mtandao wa Jinsia Tanzania (*TGNP*), Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania *(TAWLA*), Chama cha Wanawake Viongozi katika Kilimo na Mazingira (TAWLAE), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (*TAMWA*), Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (*FAWETA*), Plan International, Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA), mashirika mbali mbali pamoja na wale ambao wanafanya kazi kwa maslahi yetu kwa namna moja au nyingine.

112. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara yangu imepata ushirikiano mzuri wa wadau mbali mbali pamoja na nchi rafiki na mashirika ya kimataifa. Napenda kuzishukuru Serikali za Canada, Ireland, Italia, Netherlands, Norway na Sweden kwa kukubali kuiwezesha Wizara hii. Aidha, nayashukuru mashirika ya kimataifa ambayo ni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya watu (UNFPA), Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Maendeleo ya Wanawake (UNIFEM)

pamoja na Mashirika mengine ya ndani na nje ya nchi ambayo tumekuwa nayo karibu katika kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa.

VII. MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA

113. Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake, kwa mwaka 2005/2006 sasa naliomba Bunge lako tukufu liidhinishe matumizi ya **Shs. 8,426,084,000.** Kati ya hizo **Shs. 7,126,084,000** ni matumizi ya kawaida, ambapo **Shs. 1,912,284,000** ni mishahara (PE) na **Shs.5,213,800,000** ni kwa matumizi mengineyo (Other Charges)**.** Aidha, **Shs. 1,300,000,000** ni kwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

114. Mwisho kabisa, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba ya Wizara yangu.

115. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.